# Sheria ya Haki za Mtoto, 2009

## TAFSIRI RAHISI KWA USOMAJI WA WATOTO

hakielimu

HakiElimu
S.L.P. 79401
Dar es Salaam
Simu: (+255) 22 2151852 au 3
Faksi: (+255) 22 2152449
Barua pepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

Sheria ya Haki za Mtoto, 2009

ISBN: 9987-9331-9-8

Sheria imetafsiriwa na Mwanasheria Tadeo Mwenempazi.

**Wahariri:** Elizabeth Missokia na Elieshi Lema

**Mhariri Msaidizi:** Mtemi Zombwe.

**Michoro:** Nathan Mpangala

Kitabu haki cha sheria kimerahisisshwa na kutayarishwa na E&D Vision Publishing Ltd. kwa niaba ya HakiElimu.

Hii ni tafsiri rahisi ya sheria ya mtoto ya mwaka 2009, iliyoandaliwa na Serikali na kupitishwa na bunge mwezi Novemba 2009.

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kitabu hiki kwa minajili isiyo ya kibiashara.

# Yaliyomo

**Sura ya Kwanza**

Utangulizi ........................................................... 1

**Sura ya Pili**

Haki na Ustawi wa Mtoto........................................ 8

**Sura ya Tatu**

Kumtunza na Kumlinda Mtoto................................ 19

**Sura ya Nne**

Malezi.................................................................. 31

**Sura ya Tano**

Uzao.................................................................... 38

**Sura ya Sita**

Uangalizi na Njia ya kumtembelea Mtoto................ 42

**Sura ya Saba**

Matunzo.............................................................. 45

**Sura ya Nane**

Kulea Mtoto......................................................... 50

**Sura ya Tisa**

Kuasili Mtoto....................................................... 52

**Sura ya Kumi**

Kurithi Mali........................................................... 61

**Sura ya Kumi na Moja**

Ajira ya Mtoto........................................................ 63

**Sura ya Kumi na Mbili**

Huduma ya Msaada kwa Mtoto kutoka Mamlaka ya Serikali za Mtaa.................................................... 72

**Sura ya Kumi na Tatu**

Mtoto Mwenye Mgogoro na Sheria........................... 78

SURA 1

# UTANGULIZI

Hii ni Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009.

***Sheria ya Mtoto inahusu nini?***

Sheria hii ya mtoto inazungumzia:

- sheria za mtoto,
- haki za mtoto,
- kukuza, kulinda na kuhifadhi ustawi wa mtoto,
- masharti ya unasibishaji wa mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa,
- masuala ya kulea, kuasili na uangalizi.
- Pia inatoa maelezo na masharti yanayohusu mtoto anapokuwa katika migogoro na sheria.

Sheria hii itatumika eneo lote la Tanzania Bara. Sheria itatumika kutetea masuala yote ya kuboresha, kulinda na kuhifadhi ustawi wa mtoto pamoja na haki zake.

Sheria hii ya mtoto imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Novemba 2009.

**Dhana muhimu na maana zake:** katika Sheria hii, dhana hizi muhimu zitakuwa na maana zifuatazo:

**Makazi yaliyoidhinishwa**: maana yake ni makazi yenye kibali ambapo mtoto anaweza kupewa huduma mbadala za malezi ya familia.

**Shule iliyoidhinishwa:** ina maana ya shule iliyoanzishwa chini ya sheria hii ambapo watoto wanaweza kutunzwa na kupata elimu. Shule iliyoidhinishwa inaweza ikawa mahali popote au ikawa taasisi iliyotamkwa chini ya sheria hii.

**Elimu ya Msingi**: ina maana ya elimu rasmi inayotolewa kwa mtoto kumpatia maarifa ya msingi na muhimu. Mtoto anaweza kupatiwa elimu ya msingi wakati wowote itakapodhihirika kwamba mtoto anahitaji maarifa ya msingi.

**Kupotosha mtoto**: maana yake ni kukiuka haki za mtoto kunakosababisha madhara ya mwili, maadili au hisia. Kwa hiyo, kupotosha mtoto ni pamoja na kumpiga, kumtukana, kumtenga, kumtelekeza, kumnajisi na kumnyonya kwa kumtumikisha. Mtoto anaweza kudhurika kwa njia zote hizo wakati anapotendewa tendo asilolipenda.

**Maendeleo ya mtoto:** kuhusiana na ustawi wa mtoto, yaani wakati ambapo mtoto anajifunza kwa kufurahia na

kukua katika mazingira mazuri. Kwa hiyo, maendeleo ya mtoto ni mlolongo wa mabadiliko ambayo mtoto anaweza kupata kimwili, kiakili, kihisia na kijamii. Maendeleo ya mtoto hutokea wakati wote katika maisha yake kwa kadiri anavyohusiana na mazingira yanayomzunguka, kama shule, nyumbani, michezoni na sehemu nyingine.

**Mtoto mwenye ulemavu:** ni mtoto ambaye ana mapungufu au udhaifu wa muda mrefu au wa kudumu, wa mwili, akili, hisia au mfumo wa fahamu. Ni ulemavu ambao unamzuia asiweze kushirikiana kikamilifu na wenzake. Kuna ulemavu wa viungo vya mwili, wa akili, kama utindio wa ubongo, wa mfumo wa fahamu mfano, uziwi au upofu.

**Kamishna:** ina maana ya Kamishna wa Ustawi wa Jamii.Kamishna ni ofisa wa Serikali katika Wizara ya Wanawake, Watoto na Ustawi wa Jamii.

**Mahakama:** ina maana ya:

(a) Mahakama ya Mwanzo, Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama Kuu.

(b) Kwa madhumuni ya kuasili, Mahakama Kuu; na

(c) Kwa madhumuni ya uzawa, Mahakama ya Watoto.

**Fundistadi:** ina maana ya mtu ambaye anafundisha na kutoa maelekezo kwa mwanagenzi katika ufundi. Mwanagenzi ni mwanafunzi wa ufundi.

**Kituo cha kulea watoto wachanga**: ni kituo kilichosajiliwa kwa madhumuni ya kuwapokea na kuwalea watoto wenye umri chini ya miaka mitano, wanaofikia idadi si zaidi ya kumi wakati wa mchana, kwa malipo au pasipo malipo ya ada.

**Familia:** maana yake ni baba mzazi, mama mzazi na watoto walioasiliwa au wa damu pamoja na ndugu wa karibu, ikihusisha babu, bibi, wajomba, shangazi, binamu, wapwa ambao wanaishi katika kaya moja.

**Mtu anayefaa:** maana yake ni mtu mzima, mwenye uadilifu na mwaminifu, aliye na akili timamu, ambaye si ndugu wa mtoto lakini ana uwezo wa kulea mtoto. Huyu mtu awe amethibitishwa na Ofisa wa Ustawi wa Jamii kwamba anaweza kutoa mahali pa kukaa na kuishi kwa ajili ya malezi ya mtoto.

**Malezi au kukimu:** maana yake ni kupata upendo, mafundisho na maelekezo ya kawaida ili mtoto aishi vema, kwa kipindi cha muda mfupi. Kukimu ni kupata mahitaji ya msingi ya chakula, mavazi, mahali pa kulala na dawa mtoto anapougua. Huduma hii inaweza kutolewa kwa hiari na familia au mtu binafsi ambaye hana udugu na mtoto ili kumpatia hifadhi na ulinzi.

**Mlezi:** maana yake ni mtu anayewajibika na mwenendo wa maisha ya kila siku ya mtoto, lakini ambaye sio baba au mama mzazi. Mlezi anakuwa ameteuliwa na mahakama kwa maandishi au kwa wasia ulioachwa na mzazi au kwa amri ya mahakama. Mlezi anakuwa na mamlaka na wajibu wa kumlea mtoto na kusimamia mali na haki za mtoto.

**Kazi ya hatari**: maana yake ni kazi yoyote inayomfanya mtoto awe katika hatari ya kuumia kimwili au kiakili. Kwa mfano, kazi kwenye machimbo au kazi ya kupigana vita.

**Nyumbani:** maana yake ni mahali panapojulikana anapoishi mtoto. Nyumbani panaweza pasiwe mahali anapoishi baba na mama, au ndugu, lakini pawe mahali ambapo mzazi au mlezi aliwahi kuishi na kujulikana kwamba aliishi hapo. Kwa mfano, kama mzazi ametokea Mbeya na ana nyumba ya kuishi huko Mbeya, nyumbani panaweza kuwa Mbeya hata kama mtoto anaishi naye hapa Dar es Salaam. Isipokuwa kwamba:

(a) Kwa mzazi au mlezi mwenye makazi ya kudumu zaidi ya sehemu moja, mzazi au mlezi huyu atachukuliwa kuwa anaishi pale ambapo anapatambua kuwa ni makazi yake rasmi ya kudumu. Kwa mfano, mzazi aliye na nyumba Dar es Salaam na Mbeya, anaweza kutambua Dar es Salaam kama makazi ya kudumu. Hapo patakuwa ‘nyumbani.’

(b) Mahakama inaposhindwa kuamua makazi rasmi ya mzazi au mlezi, mahakama itaamini kuwa makazi ya mzazi au mlezi huyu ni yale yaliyopo katika eneo la Serikali ya Mtaa ambamo mtoto yumo au amepatikana;

**Taasisi**: maana yake ni makazi yaliyoidhinishwa, makazi ya kizuizi, shule zilizoidhinishwa au taasisi kwa ajili ya watoto wasio na makazi na watoto wa mitaani. Inahusisha mtu au taasisi ya malezi na udhibiti wa watoto.

**Mahakama ya watoto:** maana yake ni mahakama iliyoanzishwa kisheria kuhusika na masuala ya watoto.

**Waziri:** maana yake waziri anayehusika na masuala ya watoto.

**Rafiki wa karibu**: maana yake ni mtu anayeingilia kumsaidia mtoto kuweza kufungua shauri mahakamani. Ina maana pia ya mlezi wa muda.

**Yatima:** maana yake ni mtoto ambaye amepoteza wazazi wake wote au mzazi mmoja kwa kifo.

**Msajili mkuu:** maana yake ni msajili wa Vizazi na Vifo. Msajili Mkuu anateuliwa kulingana na sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo.

**Makazi ya kizuizi:** maana yake ni mahali ambapo mtoto hupewa makazi kwa muda wakati shauri dhidi yake likiwa linasikilizwa.

**Ndugu:** maana yake ni babu, bibi, kaka, dada, binamu, shangazi au mtu yeyote ambaye ni mhusika katika ukoo wa kidugu.

**Ofisa wa Ustawi wa Jamii:** maana yake ni ofisa wa Ustawi wa Jamii katika utumishi wa serikali.

SURA 2

# HAKI NA USTAWI WA MTOTO

***Mtoto ni nani?***

Mtoto ni mtu aliye na umri chini ya miaka kumi na nane.

**Ustawi wa mtoto;** yaani, furaha na amani kwa mtoto itapewa kipaumbele katika kutathmini mambo yote yanayomhusu mtoto, yawe yamefanywa na taasisi ya Ustawi wa Jamii ya serikali au binafsi , mahakama au vyombo vya utawala.

## Haki za Mtoto

### 1. Haki ya Kutokutengwa

Mtoto atakuwa na haki ya kuishi huru bila kuwapo na namna yoyote ya kutengwa; yaani, kuonekana kuwa hastahili kujumuika na wenzake katika kundi. Mtu yoyote haruhusiwi kumtenga mtoto kwa sababu za:

- Jinsia, rangi, umri au dini.
- Mtu hatakiwi kumtenga mtoto kwa sababu anaongea lugha tofauti.
- Mtoto hatakiwi kutengwa kwa sababu ametoa maoni tofauti ya kisiasa.




- Mtoto hatakiwi kutengwa kwa sababu ni mlemavu au kwa hali yake ya afya.
- Mtoto hatakiwi kutengwa kwa sababu ya kabila lake au mila zake.
- Mtoto hatakiwi kutengwa kwa sababu anatoka kijijini au mjini.
- Mtoto hatakiwi kutengwa kwa sababu ya hali yake ya kijamii na kiuchumi, au
- Kwa kuwa ni mkimbizi au hali yoyote nyingine.

## 2. Haki ya Jina na Utaifa

Mtoto ana haki ya kujua jina lake, utaifa, na wazazi wake waliomzaa na ukoo wa familia yake.




Mtu yeyote haruhusiwi kumnyima mtoto haki ya kujua jina lake, utaifa, na kujua wazazi wake waliomzaa na wengine katika ukoo wa wazazi wake.

## 3. Haki ya Kuishi na Wazazi au Walezi

Mtoto ana haki ya kuishi na wazazi au walezi wake.

Mtu yoyote haruhusiwi kumnyima mtoto haki ya kuishi na wazazi, walezi au familia yake. Pia, ni haki ya mtoto kukua katika malezi na mazingira ya amani.

Isipokuwa ikiamriwa na mahakama kwamba kuishi na wazazi au familia kunaweza:

(a) Kusababisha madhara makubwa kwa mtoto, hasa pale ambapo mtoto ananyanyaswa.

(b) Kumweka mtoto katika mazingira ya kutendewa vibaya;

(c) Sio vema kwa ajili ya ustawi wa mtoto, yaani, mahali ambapo mtoto haishi kwa furaha na amani.

Kwa kufuatana na sheria na taratibu zinazotumika, Mamlaka yenye uwezo, mfano, Serikali ya Mtaa, au mahakama, inaweza kuamua kwamba mtoto atenganishwe na wazazi, kwa sababu ya ustawi wake. Ikitokea hivyo, mtoto lazima apewe malezi mbadala.

## 4. Wajibu wa kumtunza mtoto

Ni wajibu wa mzazi, mlezi au mtu yeyote mwenye kumlea mtoto kutoa matunzo kwa mtoto. Wajibu huu hasa unampatia mtoto haki ya:

(a) Chakula;
(b) Malazi;
(c) Mavazi;
(d) Dawa pamoja na chanjo;
(e) Elimu na maelekezo au mafunzo;
(f) Uhuru; na
(g) Haki ya kucheza na kupumzika.

## 5. Haki ya Kupata Huduma

Mtu yeyote haruhusiwi kumnyima mtoto haki ya kupata elimu, chanjo, chakula, mavazi, malazi, huduma ya afya na dawa au kitu chochote kinachohitajika kwa ajili ya maendeleo ya mtoto.
Mtu yeyote haruhusiwi kumkatalia mtoto huduma ya dawa kwa sababu ya dini au imani yoyote ile.

## 6. Haki ya Kushiriki Michezo na Shughuli za Kiutamaduni


Mtu yeyote haruhusiwi kumnyima mtoto haki ya kushiriki katika michezo, au shughuli njema za kiutamaduni na kisanii au za starehe. Hata hivyo, ikiwa kwa maoni ya mzazi, mlezi au ndugu, kwamba kushiriki huko kutakuwa na madhara, au shughuli hizo haziendelezi ustawi wa mtoto, haki hiyo inaweza isitolewe.

Mtu yeyote haruhusiwi kumtendea mtoto mwenye ulemavu tendo lolote kwa namna isiyo ya heshima.

Watoto wenye ulemavu wa aina yoyote ile wanastahili msaada na upendo.

## 7. Haki ya Huduma ya pekee kwa Mlemavu

Mtoto mwenye ulemavu anastahili kupewa huduma ya pekee. Huduma hizi ni pamoja na: kutibiwa, kupewa nyenzo stahili kwa ajili ya kurekebisha ulemavu wake. Kwa mfano, viti na baiskeli za walemavu wa viungo, fimbo kwa kipofu au hati za alama kwa bubu. Mlemavu ana haki ya kupewa nafasi sawa katika elimu na mafunzo pale inapowezekana, ili kuendeleza vipaji vyake na uwezo wa kujitegemea.



## 8. Wajibu na Jukumu la Mzazi

Mtoto atakuwa na haki ya kuishi, kwa hadhi, heshima, uhuru, afya, kupumzika, na kupatiwa elimu na malazi kutoka kwa wazazi. Haki ya kupumzika na uhuru kwa mtoto vitategemea maelekezo na uwezo wa wazazi, walezi au ndugu.

Kila mzazi ana wajibu na majukumu kwa mtoto. Wajibu na majukumu hayo yatatekelezwa, yawe yamewekwa na sheria au vinginevyo.

Yanahusisha wajibu wa:

(a) Kumlinda mtoto dhidi ya kutelekezwa, kutengwa, kufanyiwa vurugu, kunyanyaswa, kutumiwa vibaya, na kuwa katika mazingira mabaya kimwili na kimaadili.

(b) Kutoa maelekezo, uangalizi, msaada, na hifadhi kwa ajili ya mtoto, na uhakika wa maisha na maendeleo ya mtoto.

(c) Kuhakikisha kuwa wazazi wanapokuwa mbali na mtoto, mtoto atapata uangalizi kutoka kwa mtu mwenye uwezo wa kutimiza majukumu hayo.

Wajibu na majukumu haya yanasitishwa wakati wazazi wanapotoa wajibu na majukumu hayo kwa mtu mwingine. Kutoa majukumu kutoka kwa mzazi kwenda kwa mtu mwingine kunafanywa kulingana na sheria iliyoandikwa au kwa mpango wa mila na desturi.


Iwapo wazazi waliomzaa mtoto wamefariki, wajibu wa wazazi utahamia kwa ndugu wa mzazi wa kiume au wa kike au mlezi. Watapewa wajibu na majukumu hayo kwa amri ya mahakama, au mpango wowote utakaowekwa kimila.

## 9. Haki kwa Mali za Wazazi

Mtu haruhusiwi kumnyima mtoto kumiliki na kutumia mali ya urithi kutoka kwa mzazi.

## 10. Haki ya Kutoa Maoni

Mtoto atakuwa na haki ya kutoa maoni. Hakuna mtu anayeruhusiwa kumnyima mtoto mwenye uwezo wa kutoa maoni haki ya kueleza maoni, kusikilizwa na kushiriki katika kufanya maamuzi yatakayoathiri ustawi wake.






## 11. Ajira yenye Madhara

Mtu yeyote haruhusiwi kumuajiri mtoto katika shughuli yoyote inayoweza kuwa na madhara katika maendeleo ya afya, elimu, akili, mwili na maadili yake. Kwa mfano, kazi katika viwanda vya kemikali inaleta athari kwa afya ya mtoto. Kazi ya mashambani au machimboni inayozuia mtoto kwenda shule inaathiri elimu, akili na mwili wake. Kazi ya ukahaba inaathiri maadili ya mtoto.

## 12. Kulinda Mtoto Asiteswe na Kudhalilishwa

Mtu yeyote hataruhusiwa kumfanya mtoto apate mateso, au adhabu ya kikatili, ya kinyama au afanyiwe matendo yenye kumshushia hadhi. Hii ni pamoja na desturi zozote za mila zenye kudhalilisha utu wa mtoto au zinazosababisha athari za maumivu ya mwili au akili ya mtoto. Kwa mfano, kukeketa wasichana ni kudhuru vibaya mwili, akili na hisia za mtoto wa kike. Pia, ni kitendo kinachomdhalilisha.

Hakuna adhabu kwa mtoto inayokubalika ambayo imekithiri kimatendo au kwa kiwango kulingana na umri, hali ya mwili na akili yake. Hakuna adhabu inayokubalika kwa ajili ya umri mdogo wa mtoto au vinginevyo kwa sababu mtoto hawezi kuelewa nia ya adhabu hiyo.

***Tendo lenye kudhalilisha,*** kama maneno hayo yalivyotumika katika fungu hili una maana ya tendo lililofanywa kwa mtoto kwa nia ya kudhalilisha au

kumshushia hadhi yake. Kwa mfano, kuchapa mtoto mbele ya wenzake au mbele ya umma wa watu ni tendo lenye nia ya kumdhalilisha mtoto.

***Je, adhabu ya kukiuka sheria ya haki za mtoto ni ipi?***




Mtu anayevunja sheria kama ilivyoainishwa katika sehemu hii, anatenda kosa. Baada ya kutiwa hatiani kwa kutenda kosa hilo, atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa muda usiozidi miezi sita au vyote kwa pamoja.

## Wajibu wa Jumla wa Mtoto

***Mtoto ana haki, lakini pia ana wajibu. Je, wajibu wa mtoto ni upi?***

Pamoja na haki za kulinda ustawi wa mtoto, mtoto atakuwa na wajibu na jukumu la:

(a) Kufanya kazi kwa ajili ya mshikamano wa familia.

(b) Kuwaheshimu wazazi, walezi, wakubwa wake na watu wazima muda wote na atawasaidia pale inapohitajika.

(c) Kuhudumia jamii yake na taifa lake kwa uwezo wake wote kimwili na kiakili kadiri ya umri na uwezo wake.

(d) Kutunza na kuimarisha mshikamano wa jamii na Taifa; na

(e) Kutunza na kuimarisha mambo mema katika utamaduni wa jamii na Taifa kwa ujumla katika uhusiano na wanajamii au taifa.

SURA 3

# KUMTUNZA NA KUMLINDA MTOTO

## Maana ya Kumtunza na Kumlinda Mtoto

### *Ni mtoto yupi anastahili kulindwa?*

Sheria hii inasema kwamba, mtoto anahitaji huduma na ulinzi, iwapo mtoto huyu:

(a) Ni Yatima au ametelekezwa na ndugu zake.

(b) Ameachwa au anatendewa vibaya na mtu ambaye anamtunza na kumlea mtoto au na mlezi au wazazi.


(c) Ana mzazi au mlezi ambaye hatekelezi majukumu yake kama anavyohitajika.

(d) Mtoto ni fukara.

(e) Yuko chini ya malezi ya mzazi au mlezi ambaye hafai kumlea mtoto kwa sababu ni mhalifu au ulevi.

(f) Mtoto anazurura na hana makazi au mahali pa kuishi.

(g) Ni ombaomba au anapokea misaada. Au kama mtoto amekutwa mitaani, majumbani kwa lengo la kuomba au kupokea misaada.




(h) Anaambatana na mtu ambaye anaomba au anapokea misaada, iwe kwa kuhitaji au kutohitaji, kuimba, kucheza, kuigiza, kutoa chochote kwa nia ya kuuza, au vinginevyo. Au amekutwa mitaani, majumbani kwa lengo la kuomba au kupokea misaada.

(i) Yuko chini ya malezi ya mtu fukara.

(j) Anapenda kuambatana na mtu mwenye sifa ya uhalifu au ukahaba.

(k) Anaishi katika nyumba au sehemu ya nyumba inayotumika na kahaba kwa lengo la kufanya

ukahaba. Au anaishi katika mazingira ambayo yanaweza kusababisha au yanachochea kutongozwa au kufanya ukahaba au yanaweza kuathiri maadili ya mtoto.




**Mtu asiyefaa**

***Mtu asiyefaa kumlea na kumlinda mtoto ana sifa gani?***

(i) Ni mtu ambaye amefanya kosa au amejaribu kufanya kosa kuhusiana na sheria inayozuia kusafirisha binadamu.

(a) Amekutwa akifanya jambo linaloashiria kuwa amekuwa anaomba au ameshaomba au anaombaomba kwa nia ya kutongoza kusikoendana na maadili.

(b) Ana umri chini ya miaka ishirini na moja na amehusika katika kutenda kosa la jinai.

(c) Yuko katika mazingira hatari kimwili na kimaadili. Kwa mfano, mtu anayefanya kazi akiwa uchi, mahali pa kutengenezea pombe, au mahali watu wazima wanatumia lugha chafu.

(d) Yuko chini ya matunzo ya mtu mlemavu ambaye uwezo wake unamzuia kutimiza majukumu yake kama mlezi.

(e) Yuko katika mazingira yoyote ambayo Kamishna anaweza kuamua.

(f) Mtu ambaye ni mmiliki au mkazi anayeendesha au ni msimamizi wa disko, baa au klabu ya usiku, haruhusiwi kumruhusu mtoto kuingia katika jumba hilo.

(g) Mtu haruhusiwi kumuingiza mtoto mahali popote ambapo inafanyika shughuli ya kuuza sigara, pombe, au kilevi chochote, madawa au kitu chochote kinachoweza kumlevya mtoto.

(h) Mtu anayevunja sheria katika fungu hili, anatenda kosa. Akipatikana na hatia, atawajibika kulipa faini si chini ya shilingi milioni moja lakini isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili, au yote kwa pamoja.

### Amri ya muda ya matunzo

Mahakama inaweza kutoa amri ya matunzo au amri ya matunzo ya muda baada ya maombi kupelekwa na Ofisa wa Ustawi wa Jamii kwa faida ya mtoto.

Amri ya matunzo au amri ya muda ya matunzo itamuondoa mtoto kutoka mahali alipokuwa akiteseka, au ambapo angeweza kupata madhara makubwa na kuhamisha haki za mzazi kwa Ofisa wa Ustawi wa Jamii.

Ofisa wa Ustawi wa Jamii atamtunza mtoto na kuamua mahali panapofaa mtoto kuishi ambapo panaweza kuwa:




(a) Makazi yaliyoidhinishwa.

(b) Mtu anayefaa.

(c) Mzazi, mlezi aliyethibitishwa kulingana na kanuni za matunzo ya malezi zilizotengenezwa chini ya sheria hii.

(d) Nyumbani kwa mzazi, mlezi au ndugu.

Muda wa ukomo wa amri ya malezi utakuwa miaka mitatu, au mpaka mtoto afikishe umri wa miaka kumi na nane. Hii itategemea ni muda upi utaanza kukamilika.

Mahakama inaweza kutoa amri ya ziada kwamba mzazi, mlezi au mtu yeyote atawajibika kulipa gharama za matunzo ya mtoto.

Mahakama itamteua na kuidhinisha meneja au mlezi wa taasisi au makazi yaliyoidhinishwa, kama mtu anayefaa kukabidhiwa kumlea mtoto baada ya Kamishna kutangaza kwenye gazeti la serikali.

Amri ya muda ya malezi itatolewa tu pale ambapo mtoto anapokuwa katika mateso au anaweza kupata mateso makubwa kama ilivyoainishwa katika Sheria hii.

**Amri ya Usimamizi ya Mahakama**

(i) Ofisa Ustawi wa Jamii, ataomba mahakama kutoa amri ya usimamizi au amri ya muda ya usimamizi.

***Nia ya amri ya usimamizi ni nini ?***

(ii) Amri ya usimamizi au amri ya muda ya usimamizi itakuwa na nia ya kumweka mtoto chini ya matunzo ya wazazi, walezi au ndugu. Madhumuni yake ni kuzuia mateso makubwa anayopata mtoto akiwa katika makazi ya familia.

(iii) Amri ya usimamizi au amri ya muda ya usimamizi itamweka mtoto chini ya usimamizi wa Ofisa wa Ustawi wa Jamii au mtu yeyote anayefaa. Mtu huyo atakuwa katika jamii alimo mtoto wakati akiwa chini ya malezi ya mzazi, mlezi au ndugu.

***Amri ya usimamizi itadumu kwa muda gani ?***

(iv) Muda wa ukomo wa amri ya usimamizi utakuwa mwaka mmoja au mpaka mtoto atakapofikisha umri wa miaka kumi na nane. Ofisa wa Ustawi wa Jamii, anaweza kwa ridhaa yake, akatoa maombi kuhusu kuongeza au kupunguza muda wa amri ya usimamizi.

(v) Kuongezwa kwa muda wa amri ya usimamizi kutahitaji taarifa ya maandishi ya Ofisa Ustawi wa Jamii.

(vi) Amri ya usimamizi itahitaji mtu anayeishi na mtoto:

(a) Kumtaarifu msimamizi mabadiliko yoyote ya anuani; na

(b) Kumruhusu msimamizi kumtembelea mtoto nyumbani kwa mlezi.

(vii) Maombi kwa ajili ya amri ya kumpokea mtoto kwenye makazi yaliyoidhinishwa au taasisi yatakuwa na taarifa zinazohusu:

(a) Jina, umri na anuani ya mtoto;

(b) Jinsia ya mtoto;

(c) Jina la mzazi, kama linafahamika;

(d) Utaifa;

(e) Elimu ya mtoto;

(f) Taarifa ya daktari kuhusu afya ya mtoto;

(g) Mahali alipozaliwa mtoto, kama panafahamika;

(h) Kabila; na

(i) Dini aliyozaliwa nayo.

(viii) Maombi yaliyofanywa chini ya fungu hili yatazingatia:

(a) Ustawi wa mtoto;

(b) Taarifa ya uchunguzi wa Ustawi wa Jamii; na

(c) Familia mbadala.

**Wajibu wa Ofisa wa Ustawi wa Jamii**

***Ustawi wa Jamii unamsaidiaje mtoto kuhusu malezi na usimamizi?***

(i) Wajibu wa Ofisa wa Ustawi wa Jamii kuhusu amri za malezi na usimamizi wa mtoto ni:

(a) Kutoa ushauri na mawaidha kwa mtoto na familia.

(b) Kukumbusha mara kwa mara kuhusu mipango ya baadaye ya mtoto kwa kushauriana na mtoto na wazazi au mlezi.

(c) Kupeleka maombi mahakamani ili kusitisha amri au kubadili amri kama kuna ulazima; na

(d) Kuchukua hatua za lazima ili kuhakikisha kuwa mtoto hawezi kudhurika.

**Kumtembelea nyumbani**

(i) Ofisa wa Ustawi wa Jamii ataruhusiwa na wazazi, walezi au ndugu wa mtoto kumtembelea mtoto kwenye makazi ya familia, au katika makazi yaliyoidhinishwa au taasisi, kwa vyovyote inavyowezekana.

**Sheria ya Jumla juu ya Amri**

(i) Mtoto anayekiuka amri ya mahakama na kukimbia anaweza kukamatwa na polisi na kurudishwa mahali pa malezi bila kibali cha kukamata. Kibali hiki kinatoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Ofisa Mtendaji wa Kata, au Ofisa wa Ustawi wa Jami .


(ii) Pale mtoto anapokuwa amekimbia, na mtu anayefaa wa kumlea hayuko tayari kumlea, mahakama inaweza kutoa amri nyingine ya kumweka mtoto chini ya malezi ya shule iliyoidhinishwa.

**Kuondoa Amri**

(i) Amri ya matunzo au usimamizi inaweza kuondolewa na mahakama kwa ajili ya ustawi wa mtoto, baada ya maombi kupelekwa na:

(a) Mtoto, kupitia rafiki wa karibu; yaani, ndugu au mtu anayeaminiwa na mtoto.

(b) Ofisa wa Ustawi wa Jamii;




(c) Ofisa wa Polisi;


(d) Mzazi, mlezi au ndugu wa mtoto; au

(e) Mtu yeyote mwenye majukumu ya mzazi.

**Mtoto anakuwa na haki Wazazi Wanapotengana**

***Mtoto atakuwa na haki gani wazazi wake wakitengana?***

(i) Kwa kuzingatia Sheria ya Ndoa, wazazi wanapotengana au wanapotalikiana, mtoto atakuwa na haki ya:




(a) Kupata matunzo na elimu yenye hadhi kama ilivyokuwa kabla wazazi hawajatengana au hawajatalikiana;

(b) Kuishi na mzazi ambaye, kwa maoni ya mahakama, ana uwezo wa kumlea na kumpatia matunzo kwa kiwango kinachostahili kwa ustawi wa mtoto: na

(c) Kumtembelea na kukaa na mzazi mwingine kila anapohitaji, isipokuwa kama mpango huo utaathiri ratiba ya shule au mafunzo kwa mtoto.

(ii) Kwa ajili ya kudumisha furaha na amani ya mtoto, mategemeo ni kwamba mtoto mwenye umri chini ya miaka saba ataishi na mama. Hata hivyo, jambo hilo

linaweza kupingwa. Maamuzi yatakayofanywa kwa kuzingatia pingamizi kuwa mtoto asikae na mama, mahakama itaangalia uwezekano wa kumsumbua mtoto katika maisha yake kwa kubadili makazi.

SURA 4

# MALEZI

## Majukumu ya Mzazi, Mlezi, Meneja au Mzazi Mlezi

(i) Mlezi wa makazi yaliyoidhinishwa kwa ajili ya malezi; au meneja wa taasisi au mlezi aliyepewa majukumu ya kumlea mtoto; atakuwa na majukumu ya mzazi kwa mtoto wakati wote mtoto anapokuwa chini ya uangalizi wake.

(ii) Mawasiliano ya mtoto na wazazi, ndugu au marafiki yanaruhusiwa wakati mtoto yuko katika makazi yaliyoidhinishwa, taasisi au kwa mlezi.

Kama mawasiliano hayo hayatampa mtoto furaha na amani, mawasiliano yatasitishwa.

(iii) Mlezi au meneja wa makazi yaliyoidhinishwa au taasisi au mlezi aliyekabidhiwa jukumu la kumlea mtoto, atahakikisha kuwa anaangalia kwa makini maendeleo ya mtoto, hususani afya yake na elimu kwa kipindi chote.

(iv) Mlezi au meneja wa makazi yaliyoidhinishwa au taasisi, atawasiliana na wazazi au walezi wa mtoto kuwapa taarifa ya maendeleo ya mtoto. Kwa kupitia Ofisa wa Ustawi wa Jamii, mlezi au meneja wa makazi atapanga muda wa kurudi nyumbani kwa majaribio mapema iwezekanavyo.

(v) Ofisa wa Ustawi wa Jamii anatakiwa kumtembelea mtoto anapokuwa nyumbani kwa kipindi cha majaribio. Pia atapanga mipango ya baadaye ya mtoto kwa kushauriana na meneja, mlezi au wazazi walezi.

Kipidi cha majaribio ni kipindi ambacho mtoto anarudishwa nyumbani kuangalia kama mazingira yaliyofanya aondolewe na kupelekwa kwenye makazi yaliyoidhinishwa yamebadilika kiasi cha kumfanya mtoto aishi kwa amani au furaha.

## Amri ya Kizuizi

### *Amri ya kizuizi hutolewa kwa nini?*

(i) Mahakama ya Watoto inaweza kutoa amri ya kumzuia mtu asiwe na mawasiliano na mtoto au na mtu atakayepewa jukumu la kumlea mtoto. Kizuizi hiki kitategemea mwenendo wa tabia ya mtu aliyeshindwa kutimiza majukumu ya usimamizi na matunzo ya mtoto.

(ii) Kabla ya kuweka amri ya kizuizi, mahakama inatakiwa ijiridhishe kuwa amri hiyo ni ya muhimu.

Amri ya kizuizi itawekwa kwa lengo la kumlinda mtoto na ustawi wake.

(iii) Mahakama inaweza kutamka muda ambao amri ya kizuizi itadumu.

**Utekelezaji wa Amri ya Kizuizi**

(i) Mahakama ya Watoto inaweza ikabadili au kuondoa amri ya kizuizi. Hili litafanyika kama mtu aliyetajwa katika amri ya kizuizi au mtoto anayehusika ataomba amri iondolewe au ibadilishwe.

(ii) Iwapo Ofisa wa Ustawi wa Jamii anaamini au anatuhumu kuwa mtoto anapata mateso au anaweza kupata madhara makubwa, Mahakama inaweza kutoa amri kwa Ofisa wa Ustawi wa Jamii ya kufanya upekuzi. Pia mahakama itatoa amri ya kumtoa mtoto kulingana na mwenendo wa maombi ya amri ya matunzo au amri ya usimamizi. Ofisa wa Ustawi wa Jamii ataweza kuingia katika nyumba iliyotajwa katika amri hiyo na kufanya upekuzi, kumtoa mtoto na kumpeleka mahali penye usalama. Mtoto atatolewa na Ofisa wa Ustawi wa Jamii, akiwa au hata asipokuwa na polisi.

(iii) Mtoto aliyetolewa kwa kutekeleza amri ya mahakama ya kufanya upekuzi na kumtoa, atapelekwa mahakamani ndani ya kipindi cha siku saba baada ya kutolewa.

(iv) Katika kipindi cha siku saba baada ya kumtoa mtoto kwa amri ya mahakama, Ofisa wa Ustawi wa Jamii




atampeleka mtoto mahakamani akiwa na taarifa inayozingatia matakwa ya mtoto.

(v) Pale mtoto atakapokuwa chini ya malezi ya wazazi wake, walezi au mtu yeyote anayeishi na mtoto, mtu huyo atataarifiwa mapema iwezekanavyo. Pia ataruhusiwa kuwa na mawasiliano na mtoto isipokuwa kama mawasiliano hayo yatamkosesha mtoto furaha na amani.

(vi) Mtu yeyote anayekiuka amri ya kizuizi atakuwa anatenda kosa. Akitiwa hatiani atawajibika kulipa

faini si chini ya shilingi laki tano au kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja.




## Kumtoa mtoto pasipokuwa na Mamlaka

(i) Mtu yeyote atakuwa anatenda kosa kama atamtoa mtoto ambaye yuko chini ya uangalizi wa malezi au mahali pa usalama, bila sababu ya msingi. Au akifanya hivyo bila kuwa na mamlaka au kibali cha mtu anayemtunza mtoto. Akitiwa hatiani atalipa faini si chini ya shilingi laki moja au kifungo kisichozidi miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

(ii) Ofisa wa Ustawi wa Jamii, baada ya kufanya uchunguzi, atamrudisha mtoto mahali pa usalama kama kunahitajika kufanya hivyo.

## Masharti ya Malezi

(i) Ofisa wa Ustawi wa Jamii, kwa kushirikiana na mlezi au meneja wa makazi au taasisi yaliyoidhinishwa anaweza kutoa mapendekezo kwa Kamishna kumuweka mtoto chini ya mtu anayetaka kuwa mlezi.

Hii litafanywa badala ya kumpeleka mtoto chini ya usimamizi wa makazi au taasisi iliyoidhinishwa.

(ii) Mtu anayetaka kuwa mlezi wa mtoto atapeleka maombi kwa Kamishna wa Ustawi wa Jamii.

(iii) Baada ya kupokea maombi, Kamishna, ataangalia maombi kulingana na mapendekezo yaliyofanywa na Ofisa wa Ustawi wa Jamii, mlezi na meneja.

(iv) Kamishna akiridhika kuwa mlezi mwombaji anaweza kumlea na kumtunza mtoto, na kuzingatia ustawi wake, atatoa kibali cha mtoto kuwa chini ya malezi ya mwombaji.

## Amri ya Malezi na Kuasili

***Mtoto ambaye mzazi au mlezi wake hana nia ya kumlea anaweza kufanyiwa nini ?***

(i) Mtoto ambaye yuko chini ya amri ya matunzo au usimamizi, ambaye mzazi wake, mlezi au ndugu yake, haonyeshi nia ya kudumisha furaha na amani ya mtoto, anaweza kupendekezwa aasiliwe. Mtoto ataasiliwa kwa mlezi au mahali pa malezi chini ya malezi ya mlezi wa makazi yaliyoidhinishwa.

(ii) Maombi ya amri ya malezi au usimamizi yanaweza kufanywa katika mazingira yafuatayo:

  (a) Baada ya jitihada mbalimbali za kumsaidia mtoto kufanywa na kushindikana;

(b) Madhara makubwa anayopata mtoto au anayoweza kupata yanaweza kuepukwa kwa kumuondoa mtoto mahali anapoishi.

(iii) Iwapo mtoto ataendelea kuishi mahali alipo, anaweza akapatwa na hatari kubwa.

**Lengo la Amri ya Malezi**

(i) ***Amri ya matunzo au usimamizi hutolewa kwa sababu gani ?***

(a) Kumtoa mtoto kwenye mazingira ambayo anateseka au anaweza kupata madhara makubwa.

(b) Kumsaidia mtoto na wale anaoishi nao au anapenda kuishi nao; na

(c) Kuchunguza mazingira yaliyosababisha kutoa amri na kuchukua hatua ili kupata suluhu au kuondoa tatizo ili kuhakikisha mtoto anarudi kwenye jamii.

(ii) Ofisa wa Ustawi wa Jamii ataomba amri ya matunzo au usimamizi ifanyiwe uhakiki walao mara moja kila mwaka.

SURA 5

# UZAO

## Maombi ya Nasaba

***Kama baba wa mtoto hajulikani, nani anaweza kuomba uthibitisho wa uzao?***

(i) Wafuatao wanaweza kuomba mahakamani amri ya kuthibitisha uzao wa mtoto:

(a) Mtoto;

(b) Mzazi wa mtoto;

(c) Mlezi wa mtoto;

(d) Ofisa wa Ustawi wa Jamii; au

(e) Kwa ruhusa rasmi ya mahakama, mtu yeyote mwenye kuvutiwa na mtoto.

(ii) ***Ni wakati gani maombi yanaweza kufanywa mahakamani ?***

(a) Kabla mtoto hajazaliwa;

(b) Baada ya kifo cha baba au mama wa mtoto;

(c) Kabla mtoto hajafikisha umri wa miaka kumi na nane. Inawezekana pia, kwa ruhusa rasmi ya mahakama, kuomba amri ya kuthibitisha uzao baada ya mtoto kufikisha umri wa miaka kumi na nane.

## Ushahidi wa Nasaba

(i). ***Ushahidi wa uzao wa mtoto unatokana na nini?***

(a) Ndoa yoyote iliyofungwa kwa kufuata Sheria ya Ndoa;

(b) Jina la mzazi kuingizwa katika rejesta ya vizazi inayotunzwa na Msajili Mkuu;

(c) Kufanywa kwa sherehe ya kimila na baba wa mtoto;

(d) Kutambuliwa na jamii kwa uzao huo: na

(e) Matokeo ya vipimo vya vinasaba.

## *Vipimo vya Nasaba ni nini?*

Hivi ni vipimo ambavyo vinatoa ushahidi thabiti juu ya uzao wa mtoto. Baba anayedhaniwa kuwa baba mzazi anapimwa vipimo vya nasaba ili kuwa na uhakika kwamba yeye ndiye baba mzazi. Nasaba hupatikana katika kiini cha seli hai na huwa na taarifa za urithi kutoka kwa mzazi kwenda kwa mtoto. Taarifa za nasaba ndizo pekee zenye kutoa ukweli usiopingika kuhusu uzao wa mtoto.




## Vipimo vya Kidaktari

(i) Mahakama inaweza kutoa amri, kwa anayesemekana kuwa ni baba mzazi wa mtoto, kupeleka vipimo vya kidaktari. Kwa kutegemea na ushahidi utakaopatikana kutokana na vipimo, mahakama itatoa amri kama inavyoona inafaa.

(ii) Pamoja na vipimo vya kidaktari, pale ambapo ushahidi wa mama au ushahidi mwingine wowote unaojitegemea haulingani/haufanani na ushahidi uliopatikana kutokana na vipimo, mahakama yenyewe, inaweza kuamuru vipimo vya vinasaba

vifanywe kwa nia ya kuthibitisha baba mzazi wa mtoto.

Au, maombi ya vipimo vya kinasaba yanaweza kupelekwa mahakani.

(iii) Mahakama itaamua na kutoa amri nani atalipia gharama kuhusiana na vipimo vya vinasaba.

(iv) Pale mahakama inapotoa amri kuhusu baba mzazi, baba huyu atachukua majukumu kwa mtoto kama vile anavyowajibika kwa mtoto aliyezaliwa ndani ya ndoa. Mtoto naye, kwa kuzingatia dini ya baba mzazi, atakuwa na haki zote kutoka kwa baba pamoja na haki ya urithi.

SURA 6

# UANGALIZI NA NJIA YA KUMTEMBELEA MTOTO

***Nani anaweza kuwa mwangalizi wa mtoto?***

(i) Mzazi, mlezi au ndugu anayemtunza mtoto anaweza kuomba mahakamani kuwa mwangalizi wa mtoto.

(ii) Mahakama inaweza kutoa amri ya kuishi na mtoto kwa mwombaji kuwa mwangalizi, kwa masharti itakayoona yanafaa. Hili litategemea mwenendo wa maombi ya kuthibitisha uzao wa mtoto.

(iii) Mahakama inaweza, wakati wowote, kufuta amri ya kuishi na mtoto kama mwangalizi kwa mtu na kumpatia mtu mwingine majukumu hayo. Majukumu hayo yanaweza pia yakapatiwa makazi yaliyoidhinishwa au taasisi, kama mahakama ikiona ni lazima.

(iv) Katika kufikia maamuzi ya kutoa amri ya kuwa mwangalizi wa mtoto au kufuta amri hiyo, mahakama itazingatia kwanza furaha na amani ya mtoto.

**Kumtembelea mtoto**

Mzazi, mlezi au ndugu ambaye amefutiwa amri ya kuwa mwangalizi wa mtoto anaweza kuomba mahakamani kupata nafasi ya kumtembelea mtoto kwa vipindi maalumu.

**Uamuzi juu ya Kumtembelea Mtoto**

(i) Mahakama itazingatia furaha na amani ya mtoto na umuhimu wa mtoto kuwa na mama yake wakati inapotoa amri ya uangalizi wa mtoto na kumtembelea mtoto.

(ii) ***Wakati wa kutoa amri ya uangalizi, mahakama inazingatia nini?***

(a) Haki za mtoto;

(b) Umri na jinsia ya mtoto;

(c) Kama inafaa mtoto kuwa na wazazi, isipokuwa kama mtoto atanyimwa haki zake za kuwa na wazazi. Au, kama wazazi wataendelea kuzivunja haki za mtoto.

(d) Maoni ya mtoto, kama maoni hayo yametolewa kwa uhuru.

(e) Kwamba inafaa kuwaweka ndugu pamoja;

(f) Hitaji la kuwepo mwendelezo wa matunzo na udhibiti wa mtoto; na

( g) Jambo lolote ambalo mahakama itaona linafaa.

**Kumuondoa Mtoto Kinyume cha Sheria**

(i) Mtu yeyote atakuwa anatenda kosa, kama atamwondoa mtoto kutoka kwa mtu anayeishi naye kihalali, makazi yaliyoidhinishwa au taasisi, kinyume cha sheria.

SURA 7

# MATUNZO

***Ni nani wanaweza kuomba kumtunza mtoto?***

(i) Watu wafuatao wanaweza kuomba mahakamani amri ya kukimu mtoto:-

(a) Mzazi wa mtoto;

(b) Mlezi wa mtoto

(c) Mtoto mwenyewe, kwa kumtumia rafiki wa karibu;

(d) Ofisa wa Ustawi wa Jamii

(e) Ndugu wa mtoto.

(ii) Maombi ya kukimu mtoto yanaweza kufanywa dhidi ya mtu yeyote anayestahili kumtunza mtoto, au kwa madhumuni ya kuchangia kwa ajili ya ustawi na matunzo ya mtoto.

**Amri ya kukimu mtoto dhidi ya anayesemekana ni baba mzazi wa mtoto**

(i) Maombi ya amri ya kukimu mtoto yanaweza kufanywa mahakama ni dhidi ya baba anayesemekana kuwa baba mzazi wa mtoto.

***Maombi ya kukimu yanaweza kufanywa na nani?***

(a) Na Mama anayetarajia kujifungua wakati wowote kabla ya mtoto kuzaliwa;

(b) Na mzazi ambaye amri ya uzao imetolewa dhidi yake na mahakama.

***Ni wakati gani maombi ya kukimu mtoto yanaweza kufanywa?***

(c) Wakati wowote ndani ya miezi ishirini na nne (miaka miwili) baada ya kuzaliwa mtoto;

(d) Wakati wowote baada ya mtoto kuzaliwa, na baada ya kuthibitisha kwamba mwanamume anayesemekana kuwa ni baba wa kibaiolojia wa mtoto amelipa hela kwa ajili ya kumkimu mtoto ndani ya miezi ishirini na nne baada ya mtoto kuzaliwa.

(e) Wakati wowote ndani ya miezi ishirini na nne baada ya baba mzazi wa mtoto kurudi ndani ya Tanzania Bara, baada ya kuthibitika kwamba aliacha kuishi Tanzania kabla au baada ya mtoto kuzaliwa.

(ii) Mahakama itakataa kutoa amri ya kukimu mtoto chini ya kifungu cha (i) isipokuwa ikiridhika kwamba:

(a) Kuna sababu ya maana kuamini kwamba mwanamume anayesemekana ni baba wa

mtoto, kweli ni baba wa mtoto, na kwamba maombi ya matunzo yamefanywa kwa nia njema wala si kwa lengo la kuogofya na kulazimisha malipo kwa nguvu; na

(b) Mwanamume anayesemekana kuwa ni baba wa mtoto ameombwa na mwombaji au mtu mwingine kwa niaba ya mwombaji kutoa matunzo ya mtoto naye amekataa au amepuuzia kutoa matunzo au ametoa kidogo.

## Uamuzi kwa ajili ya Amri ya Kukimu Mtoto

(i) Mahakama itaangalia mambo yafuatayo inapotoa amri ya malipo ya matunzo:

(a) Kipato na utajiri wa wazazi wote wa mtoto au wa mtu ambaye kisheria anawajibika kutoa matunzo ya mtoto;

(b) Kama kipato cha mtu anayewajibika kutoa matunzo ya mtoto kikididimia.

(c) Majukumu ya kifedha mtu aliyonayo kwa matunzo ya watoto wengine;

(d) Gharama za maisha za eneo ambapo mtoto anaishi; na

(e ) Haki za mtoto chini ya sheria hii.

(ii) Mtu yeyote ambaye anamlea mtoto anayehusika na amri ya kukimu mtoto anastahili kupokea na kusimamia amri ya mahakama ya kukimu mtoto.




(iii) Pale mzazi, mlezi au mtu yeyote anayemlea mtoto anapopoteza sifa za kuwa mtu anayefaa, mahakama iliyopo katika eneo analoishi mtoto inaweza kumteua mtu mwingine awe mlezi wa mtoto. Mtu huyu atasimamia amri ya kukimu mtoto na atatimiza majukumu yake kama vile aliteuliwa na mahakama tangu awali.

## Muda wa Amri ya Kukimu Mtoto

(i) Amri ya kukimu mtoto iliyotolewa na mahakama itadumu mpaka mtoto anapofikisha umri wa

miaka kumi na nane. Au itadumu hadi apate ajira inayompatia kipato. Au amekufa kabla ya kutimiza umri wa miaka kumi na nane.

### Mwendelezo wa Amri ya Kukimu

(i) Mahakama inaweza kuendelea kutekeleza amri ya kukimu mtoto baada ya mtoto kutimiza umri wa miaka kumi na nane. Amri ya kukimu itaendelea kama mtoto bado anaendelea na masomo au mafunzo, licha ya muda wa ukomo kama ilivyoainishwa katika sheria hii.

(ii) Maombi chini ya fungu hili yanaweza kuletwa na mzazi wa mtoto, mtu yeyote anayemlea mtoto, au mtoto mwenyewe.

(iii) Mtu yeyote mwingine anaweza kupeleka maombi mahakami kutekeleza amri ya kukimu mtoto ndani ya siku arobaini na tano baada ya amri kutolewa au kuwa tayari kwa utekelezaji.

### *Je, mzazi ambaye haishi na mtoto anaruhusiwa kumwona?*

Mzazi ambaye haishi na mtoto ataruhusiwa kumtembelea mtoto. Jambo hili halizuiwi na amri ya kuthibitisha uzao, uangalizi, kumtembelea mtoto au ya kukimu mtoto iliyotolewa na mahakama dhidi yake.

SURA 8

# KULEA MTOTO

***Nani anaweza kuwa mlezi?***

(i) Mtu yeyote mwenye umri juu ya miaka ishirini na moja, mwenye maadili mema na tabia njema, anaweza kuwa mlezi wa mtoto.

(ii) **Mlezi**, kama ilivyotumika katika sehemu hii, ni mtu ambae siyo mzazi wa mtoto lakini ana hiari na uwezo wa kumtunza na kumkimu mtoto.

(iii) Kamishna anaweza kumweka mtoto chini ya mlezi pale:

(a) Mtoto anapopelekwa katika makazi yaliyoidhinishwa au taasisi chini ya amri ya usimamizi;


(b) Mapendekezo yanapofanywa na Ofisa wa Ustawi wa Jamii kwamba makazi yaliyoidhinishwa au taasisi ni mahali panapomfaa mtoto; au

(c) Mtoto anapokuwa amewekwa na mtu yeyote katika makazi yaliyoidhinishwa au taasisi.

(iv) Maombi ya kumlea mtoto yatafanywa kwa Kamishna, ambaye atayapeleka kwa Ofisa wa

Ustawi wa Jamii, mlezi au mtu aliye na mamlaka katika makazi yaliyoidhinishwa.

(v) Mlezi ambaye mtoto amewekwa chini ya matunzo na malezi yake atakuwa na majukumu ya kumlea na kumkimu mtoto sawa na majukumu aliyonayo mzazi wa mtoto.




(vi) Mtoto aliyewekwa chini ya malezi atakuwa na haki ya kuabudu kulingana na imani ya dini yake wakati alipozaliwa.

(vii) Mlezi anayekiuka sheria kama ilivyoainishwa sehemu hii atakuwa ametenda kosa chini ya sheria hii.

SURA 9

# KUASILI MTOTO

## Kutoa Amri ya Kuasili

### *Maombi ya kuasili yanafanywa wapi?*

(i) Kwa kuzingatia sheria kama ilivyoainishwa katika Sheria hii:

(a) Maombi ya kuasili mtoto yanaweza kufanywa Mahakama Kuu;

(b) Maombi kwa ajili ya "**kuasili kwa wazi**" yatafanywa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi au Mahakama ya Wilaya.

(ii) Baada ya kupokea maombi, Mahakama inaweza kutoa amri ya kuruhusu maombi ya kuasili au kuasili kwa wazi kulingana na Sheria hii.

(iii) Maana ya **kuasili kwa wazi**" kama ilivyotumika katika sheria hii, ni kuasili mtoto kunakofanywa na ndugu.

***Ni nani anaweza kuomba kuasili?***

**Maombi ya kuasili**

(i) Maombi ya amri ya kuasili yanaweza kufanywa kwa pamoja na

 (a) Mume na mke; au

 (b) Mama au baba wa mtoto peke yake au pamoja na mwenzi wake.




(ii) Kuhusu maombi ya kuasili kwa wazi, maombi hayo yanaweza kufanywa na ndugu wa mtoto.

## Ridhaa ya Wazazi na Walezi

(i) Amri ya kuasili itatolewa tu kunapokuwa na ridhaa ya wazazi au walezi wa mtoto.

(ii) Mahakama inaweza kutohitaji ridhaa ya wazazi, walezi au ndugu wa mtoto kama itaridhika kwamba:

(a) Wazazi, walezi au ndugu wamemtelekeza mtoto au wamekuwa wakimtendea mtoto vibaya kwa muda mrefu.

(b) Au kama mtu hawezi kupatikana au hana uwezo wa kutoa ridhaa.

(c) Au kama hakuna sababu ya maana ya kutokutoa ridhaa.

(iii) Mzazi yeyote, mlezi au ndugu wa mtoto ambaye anahusika katika maombi ya kuasili au ametoa ridhaa kwa ajili ya amri ya kuasili hatastahili kumtoa mtoto kutoka kwa mwombaji. Itakuwa hivyo tu kama ana kibali cha mahakama na itakuwa kwa manufaa ya mtoto.

## Amri ya kuasili

***Je, mtoto aliyeasiliwa ana haki ya kupewa taarifa ya uasili?***

(i) Mzazi aliyeasili atamfahamisha mtoto aliyeasiliwa kwamba ameasiliwa. Atamfahamisha pia kuhusu nasaba yake. Lakini, taarifa hii itatolewa kama:

(a) Ni kwa ajili ya manufaa ya mtoto; na

(b) Mtoto ana umri angalau wa miaka kumi na nane.

(ii) Mtu mwingine hana ruhusa ya kutoa taarifa kwamba mtoto ameasiliwa isipokuwa mzazi wa kuasili.

(iii) Mtu yeyote anayekiuka kifungu hiki anatenda kosa. Akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya si chini ya shilingi mia moja elfu, lakini isiyozidi shilingi milioni mbili au kifungo cha muda usiozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

**Maombi yaliyofanywa na Mtu Asiyekuwa Mkazi**

(i) Katika maombi ya kuasili yaliyofanywa na mwombaji ambaye ni raia wa Tanzania, lakini haishi ndani ya Tanzania, mahakama itajiridhisha kwamba kuna taarifa za kutosha kuweza kufanya maombi, kisha itatoa amri ya muda.

Vilevile, kama maombi ya pamoja yamefanywa, na mmoja wa waombaji si mkazi wa Tanzania, mahakama itajiridhisha kwamba kuna taarifa za kutosha kuweza kufanya maombi, kisha itatoa amri ya muda.

(ii) Mahakama itajiridhisha kwamba kuna taarifa za kutosha kutoka kwa mamlaka inayotambulika kule mwombaji anakoishi na kwenye nchi yake ya asili, ndipo itoe amri ya muda au amri ya kuasili.

**Watoto ambao waliasiliwa kabla**

(i) Amri ya kuasili au amri ya muda inaweza kufanywa kwa ajili ya mtoto ambaye ameshaasiliwa na wazazi wa kuasili . Kama wazazi wa kuasili wa awali bado wako hai, watachukuliwa kuwa ni wazazi au walezi wa mtoto kwa lengo la kuasili kunakofuata.

**Athari za Kuasili kwa haki za Mzazi**

(i) Wakati amri ya kutoa amri ya kuasili:

(a) Haki, wajibu na majukumu yanayotokana na kuasili yana ukomo. Haya ni pamoja na yale yanayotokana na sheria za mila na desturi za wazazi wa mtoto, au mtu yeyote anayehusiana na mtoto.

(b) Haki, wajibu na majukumu ya wazazi vitakuwa chini ya mzazi wa kuasili ambaye anachukua nafasi ya mzazi wa mtoto. Hii inajumuisha majukumu yote kuhusu uangalizi, kukimu na elimu ya mtoto, kama vile mtoto alizaliwa na wazazi wa kuasili kisheria katika ndoa yao, na hakuwa mtoto wa mtu mwingine .

(ii) Pale ambapo amri ya kuasili imetolewa kwa mume na mke kwa pamoja, wote kwa pamoja watachukua majukumu ya wazazi kama vile wamemzaa mtoto wao wenyewe kiasili kama mume na mke.

## Kuasili na Sheria za Kimila

(i) Mtoto wa kuasili atakuwa chini ya sheria za kimila kama vile alikuwa mtoto wa kuzaliwa wa wazazi wa kuasili kama wazazi wa kuasili wako chini ya sheria za kimila.

## Usajili wa Watoto Walioasiliwa

(i) Amri ya kuasili iliyotolewa na mahakama itakuwa na maelekezo kwa Msajili Mkuu kuweka kumbukumbu katika Rejesta ya Watoto Walioasiliwa.

(ii) Kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya kumbukumbu ya rejesta, ambapo:

(a) Tarehe halisi ya kuzaliwa mtoto haijathibitika kuweza kuiridhisha mahakama, mahakama itaamua tarehe inayoelekea kuwa tarehe ya kuzaliwa kwa mtoto. Tarehe hiyo itatajwa kwenye amri.

(b) Jina au ubini litakalotumika kwa mtoto likiwa tofauti na lile la awali, jina jipya litatajwa kwenye amri badala ya jina la zamani.

(c) Nchi aliyozaliwa mtoto haijathibitika kuweza kuiridhisha mahakama, taarifa za nchi hiyo zinaweza kuachwa katika amri ya kuasili. Nchi haitawekwa pia kwenye Rejesta ya Watoto Walioasiliwa.

(iii) Kwa mtoto ambaye alikuwa hajaasiliwa, maelezo ya kwamba "Ameasiliwa" yatatolewa kwa Msajili Mkuu na kuwekwa kwenye taarifa za Rejesta ya Vizazi. Hili litafanyika baada ya mahakama kupokea maombi ya amri ya kuasili na kujiridhisha kwamba taarifa zinaendana na zile zilizo kwenye Rejesta ya Vizazi.

(iv) Pale ambapo amri ya kuasili imetolewa na mahakama chini ya sheria hii, mahakama itawasilisha maelekezo kwa Msajili Mkuu. Baada ya kupokea mawasiliano hayo,Msajili Mkuu atawezesha maelekezo yaliyoko kwenye amri ya mahakama yatekelezwe yote. Neno "Ameasiliwa" litawekwa kwenye Rejesta ya Vizazi na katika Rejesta ya Watoto Walioasiliwa.



## Kuasiliwa na Mtu Asiye Raia

***Je, mtoto anaweza kuasiliwa na mtu ambaye sio Mtanzania?***

(i) Mtu yeyote ambaye siyo raia wa Tanzania anaweza kuasili mtoto ambaye ni Mtanzania.

Hilo linawezekana kama:

(a) Mtoto hawezi kuwekwa chini ya malezi au kwenye familia ya kuasili. Au kama mtoto

hawezi kutunzwa katika hali ambayo inafaa kwa ajili ya ustawi wake akiwa Tanzania.

(b) Mtu anayetaka kuasili ameishi Tanzania kwa muda wa miaka mitatu mfululizo;

(c) Amemlea mtoto kwa muda wa miezi mitatu chini ya usimamizi wa Ofisa Ustawi wa Jamii;




(d) Hana historia ya kutenda makosa ya kijinai katika nchi aliyotoka au nchi nyingine yoyote;

(e) Amependekezwa kuwa anafaa kumuasili mtoto kutoka kwa Ofisa wa Ustawi wa Jamii. Au kama amependekezwa na mamlaka yenye uwezo katika nchi ambako anaishi.

(f) Ameiridhisha mahakama kwamba nchi alikotoka inaheshimu na inatambua amri ya kuasili.

(ii) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (i) , mahakama inaweza kutoa amri ya kuasili kama ni kwa ajili ya manufaa ya mtoto.

(iii) Kwa ajili ya maombi ya kuasili ya mtu ambaye sio raia wa Tanzania, Ofisa Ustawi wa Jamii atatakiwa kufanya uchunguzi. Ofisa wa Ustawi wa Jamii atatoa ripoti ya uchunguzi wa kijamii ili kuisaidia mahakama kufanya uamuzi kuhusu maombi.

(iv) Mahakama inaweza kutoa amri ya ziada kuhusiana na maombi ya kuasili ya mtu asiye raia wa Tanzania:

(a) Kumtaka Ofisa wa Ustawi wa Jamii kuwakilisha maslahi ya ustawi wa mtoto;

(b) Kumtaka Ofisa wa Ustawi wa Jamii kuandaa ripoti ya uchunguzi wa kijamii ili kuisaidia mahakama kufanya maamuzi, iwapo amri ya kuasili itakuwa kwa manufaa ya mtoto au la;

(c) Suala lolote ambalo mahakama inaweza kuamua.

SURA 10

# KURITHI MALI

## Kugawa Mali bila Wasia

***Je, mtoto aliyeasiliwa atarithi mali zipi?***

(i) Pale mzazi wa kuasili anapofariki bila kuacha wasia, mali zake zinakuwa mali za mtoto wa kuasili, kama vile mtoto amezaliwa na wazazi wa kuasili.

(ii) Kwa ajili ya kuondoa utata, mtoto wa kuasili hatastahili kurithi mali kama wazazi wake wa kibaiolojia wakifa bila kuacha wasia.

## Kugawa Mali kwa Wasia

(i) Mgawanyo unaofanywa baada ya tarehe ya amri ya kuasili, iwe mali halisi au binafsi, iwe au isiwe kwa maandishi, itazingatia:

(a) Maelezo yoyote yenye marejeo, yaliyo wazi au kwa kuhisi, yanayohusu mtoto wa mzazi wa kuasili, yanamhusu pia mtoto wa kuasili, isipokuwa kama itaonyeshwa vinginevyo.

(b) Pale ambapo mgao ulifanywa na mzazi wa kuasili kabla ya tarehe ya kutolewa amri ya kuasili, na mtoto wa kuasili hakutajwa katika mgao huo, mtoto wa kuasili anaweza kuomba mahakamani ili mgao huo uweze kubadilishwa, ili naye ahusishwe katika mgao.

(c) Marejeo yoyote kwa wazazi wa mtoto wa kuasili katika wasia, hayatatafsiriwa kumhusisha mtoto aliyeasiliwa, isipokuwa kama kutakuwa na nia ya kufanya hivyo.

(d) Marejeo yoyote kwa ndugu wa mzazi wa kuasili, hayatatafsiriwa kuwa yanarejea kwa mtu huyo kama vile ni ndugu wa mtoto aliyeasiliwa, isipokuwa kama kutakuwa na nia ya kufanya hivyo.

(ii) Mgao katika wasia unaofanywa kabla ya tarehe ya amri ya kuasili hautachukuliwa kama vile umefanywa baada ya tarehe ya amri ya kuasili. Kiambatisho cha wasia cha tarehe kabla ya amri ya kuasili hakiwezi kukubalika.

(iii) M**gao**, lina maana ya kuhamisha masilahi katika mali kwa hati yoyote, iwe kwa watu walio hai, au kwa wasia, ikiwa ni pamoja na kiambatisho cha wasia.

SURA 11

# AJIRA YA MTOTO

## Haki ya Mtoto Kufanya Kazi

(i) Mtoto atakuwa na haki ya kufanya kazi nyepesi.

(ii) Pamoja na kwamba mtoto ana haki ya kufanya kazi nyepesi, umri wa chini wa kuajiri mtoto utakuwa miaka kumi na nne.

### *Kazi nyepesi ni zipi?*

(iii) ***Kazi nyepesi***" itahusisha kazi ambayo haiwezi kuwa na madhara kwa afya ya mtoto, au kwa maendeleo yake. Kazi hiyo haitamzuia au haitaathiri mahudhurio ya mtoto ya shule, kushiriki katika shughuli za kujiendeleza kiufundi au programu ya mafunzo au uwezo wa mtoto kunufaika na kazi za shule.

## Kukataza Kazi za Kiunyonyaji

(i) Mtu hataruhusiwa kumuajiri au kumshughulisha mtoto katika aina yoyote ya kazi itakayomnyonya mtoto.

(ii) Bila kupingana na kifungu hiki cha sheria, kila mwajiri atahakikisha kuwa kila mtoto aliyeajiriwa kihalali na kulingana na sheria hii, analindwa. Mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya kutengwa au matendo yoyote yanayoweza kuwa na athari mbaya kwake kwa kuzingatia umri na uwezo wake.

(iii) ***Nini maana ya kazi za kinyonyaji?***

Kazi itakuwa ni ya kinyonyaji iwapo:

(a) Inamnyima mtoto kuwa na afya njema au maendeleo;



(b) Ni ya muda zaidi ya saa sita kwa siku;

(c) Haifai kwa umri wake; au

(d) Mtoto hapati malipo ya kutosha

(iv) Mtu yeyote anayevunja sheria katika kifungu hiki anatenda kosa. Akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja au kutumikia kifungo kwa muda wa miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

***Ni katika kazi zipi mtoto hawezi kuajiriwa?***

**Kukataza Kazi za Usiku**

(i) Bila kupingana na sheria hii, mtoto hataajiriwa au kuhusishwa katika mkataba wa huduma ambayo itamuhitaji mtoto afanye kazi usiku.

(ii) "**Kazi ya usiku**" ni kazi inayohusu utendaji unaohitaji mtoto awe kazini kati ya saa mbili jioni na saa kumi na mbili asubuhi.

(iii) Mtu yeyote anayevunja sheria katika kifungu hiki anatenda kosa. Akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja au kutumikia kifungo kwa muda wa miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

## Kukataza Ajira ya Lazima

(i) Mtu yeyote atakayemshawishi, atakayempeleka, atakayemtaka au atakayemlazimisha mtoto kufanya kazi kwa lazima anatenda kosa.

(ii) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, '***ajira ya muda***" inahusisha kazi ya kitumwa au kazi yoyote inayofanyika kwa vitisho vya adhabu. Ajira ya muda haihusishi kazi za kawaida za kijamii, kazi ndogondogo za huduma kwa jamii zinazofanywa na wanajumuiya kwa manufaa ya jamii.

(iii) Mtu yeyote anayevunja sheria katika kifungu hiki anatenda kosa. Akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili au kutumikia kifungo cha muda wa miezi sita au vyote kwa pamoja.

## Haki ya Kulipwa Ujira

(i) Mtoto ana haki ya kulipwa ujira sawa na thamani ya kazi aliyofanya.

(ii) Licha ya sheria kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Kazi na Uhusiano wa Kikazi, mwajiri yeyote ambaye anakiuka sheria katika kifungu hiki anatenda kosa.

**Ajira ya Hatari**

(i) Siyo halali kisheria kumuajiri au kumhusisha mtoto kwenye kazi ya hatari.

***Ajira za hatari ni zipi?***

(ii) ***Kazi ya hatari*** ni kazi yoyote inayoweza kuleta hatari kwa afya, usalama na maadili ya mtoto.

(iii) Kazi ya hatari itahusisha:-

(a) Kwenda baharini;

(b) Kufanya kazi migodini au kuchimba na kupasua kokoto;



(c) Kubeba mizigo mizito;

(d) Kufanya kazi katika viwanda vya uzalishaji ambako kemikali zinatengenezwa au kutumika;

(e) Kufanya kazi sehemu ambako mashine zinatumika; na

(f) Kufanya kazi sehemu za baa, hoteli au sehemu nyingine za starehe.

(iv) Pamoja na kwamba kazi za hatari zimeainishwa na kuzuiwa, sheria yoyote iliyoandikwa inayosimamia mafunzo inaweza kumruhusu mtoto:

(a) Kuingia katika merikebu ili ahudhurie mafunzo kama sehemu ya mafunzo ya mtoto;

(b) Katika kiwanda au mgodi, kama kazi ni sehemu ya mafunzo ya mtoto;

(c ) Katika sehemu yoyote ya kazi kwa masharti kwamba afya, usalama, na maadili ya mtoto vitalindwa na mtoto amepata au anapata maelekezo maalumu, au mafunzo yanayoendana na kazi au shughuli hiyo.

## Kumtumia Mtoto kwa Shughuli za Kikahaba

(i) Mtoto hataajiriwa katika kazi yoyote au biashara inayomweka mtoto katika mazingira ya ngono, iwe kwa malipo au la;

(ii) Kwa kuondoa utata, itakuwa ni kukiuka sheria kwa mtu yoyote kutumia:

   (a) Ushawishi au kumlazimisha mtoto ashiriki katika vitendo vya ngono;

   (b) Watoto katika vitendo au shughuli zozote za umalaya;

   (c) Watoto katika kutengeneza picha au maandishi yenye kutia ashiki.

(iii) Mtu yeyote anayevunja sheria katika kifungu hiki anatenda kosa. Akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kutumikia kifungo kwa muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi miaka ishirini au vyote kwa pamoja.

***Sheria juu ya kazi za hatari itatumika sehemu gani?***

(i) Kwa kuzuia utata, sehemu hii itatumika kwa ajira katika sekta rasmi na isiyo rasmi.

(ii) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (i), Ofisa wa Kazi, katika muda muafaka, ataingia katika nyumba au sehemu ya nyumba na kufanya ukaguzi kama ataona ni lazima, ili kujiridhisha kwamba sheria katika sehemu hii inatekelezwa.

(iii) Neno ***"nyumba"*** lina maana ya nyumba, shirika, kampuni, ofisi, uwanja, shamba, eneo; na inahusisha chombo, merikebu, gari na ndege.

## Usajili wa Mtoto katika Sehemu za Kazi

***Je, taarifa zinazohusu mtoto katika sehemu ya kazi ni zipi?***

(i) Mwajiri, katika sehemu za kazi, atatunza rejesta ya watoto walioajiriwa naye, tarehe za kuzaliwa kwao, kama zinafahamika au umri unaodhaniwa kuwa ndio umri wao, kama tarehe zao za kuzaliwa hazijulikani.

(ii) Shughuli za kikazi ni shughuli nyingine ambazo si za kibiashara au kilimo. Shughuli za kikazi zinajumuisha:

(a) Migodi, machimbo ya mawe, na kazi nyingine za kuchimba madini kutoka ardhini.

(b) Shughuli ambazo kutokana nazo, vitu mbalimbali vinatengenezwa, vinabadilishwa, vinasafishwa, vinakarabatiwa, vinapambwa, vinaboreshwa, vinatwaliwa kwa kuuzwa, vinavunjwa au kuharibiwa, au ambako vitu vinabadilishwa. Zinajumuisha shughuli za kujenga merikebu au shughuli za kufua, kubadili na kusambaza umeme au nishati ya aina yoyote.

(c) Shughuli za kusafirisha abiria au bidhaa kwa barabara au reli pamoja na kushughulikia bidhaa katika gati, kikwezo, ghala na uwanja wa ndege.

## Utekelezaji wa Sheria

***Sheria ya ajira kwa watoto inafuatiliwa na nani? Wakati gani?***

(i) Ofisa wa Kazi atafanya uchunguzi wowote kama anaona ni lazima ili kujiridhisha kwamba sheria katika sehemu hii kuhusu ajira ya watoto zinatekelezwa kwa hakika.

(ii) Ofisa wa Kazi anaweza kumusaili mtu yeyote kama ni lazima.

(iii) Pale ambapo Ofisa wa Kazi kwa busara zake ameridhika kwamba sheria katika kifungu hiki haitekelezwi, atatoa amri ya kutokutekelezwa kwa sheria katika ajira. Ofisa wa Kazi atapeleka ripoti kwa Ofisa Ustawi wa Jamii na kituo cha polisi kilicho karibu. Ofisa wa Ustawi wa Jamii na polisi watafanya upelelezi na kuchukua hatua zinazofaa ili kumlinda mtoto.

SURA 12

# HUDUMA YA MSAADA KWA MTOTO KUTOKA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MTAA

## Wajibu wa Mamlaka ya Serikali za Mtaa

### *Mtoto anafanyiwa nini na Mamlaka ya Serikali za Mtaa?*

(i) Mamlaka ya Serikali ya Mtaa itakuwa na wajibu wa kulinda na kukuza ustawi wa mtoto katika eneo la mamlaka hiyo.

(ii) Ofisa wa Ustawi wa Jamii katika mamlaka ya Serikali ya Mtaa atatimiza kazi zake kuhusiana na ustawi wa mtoto. Atasaidiwa na maofisa wa Serikali ya Mtaa kama mamlaka inavyoweza kuamua.

(iii) Mamlaka ya Serikali ya Mtaa kwa kupitia Ofisa wa Ustawi wa Jamii itatoa ushauri kwa wazazi, walezi na ndugu na watoto kwa madhumuni ya kukuza upatano kati yao.

(iv) Mamlaka ya Serikali ya Mtaa itakuwa na wajibu wa kutunza Rejesta ya Watoto wenye kuweza kudhurika zaidi katika eneo lake. Watatoa msaada pale inapowezekana ili kuwawezesha watoto kukua kwa hadhi na heshima baina ya watoto wengine, kukuza vipaji na uwezo wa kujitegemea.

(v) Kila mamlaka ya Serikali ya Mtaa katika eneo lake itatakiwa kutoa msaada na mahali pa kuishi kwa mtoto anayeonekana kwa mamlaka hiyo kuhitaji msaada. Mtoto atakayehitaji msaada anaweza kuwa amepotea au kutelekezwa au anatafuta hifadhi.


(vi) Kila mamlaka ya Serikali ya Mtaa itafanya kazi na polisi kwa kila jitihada kuwatafuta wazazi, walezi au ndugu wa mtoto aliyepotea, aliyetelekezwa na kumrudisha mtoto mahali alipokuwa akiishi. Serikali ya Mtaa ikishindwa kuwapata wazazi au ndugu, itapeleka suala hili kwa Ofisa wa Ustawi wa Jamii.

(vii) Ofisa wa Ustawi wa Jamii na polisi katika eneo la mamlaka ya Serikali ya Mtaa watapeleleza kesi zote za kukiuka au kuvunjwa kwa haki za watoto.

## Taarifa ya Kuvunjwa kwa Haki za Watoto

***Mwanajumuiya katika jamii ana wajibu gani kwa mtoto?***

(i) Mwanajumuiya yeyote ana wajibu wa kutoa taarifa kwa mamlaka ya Serikali ya Mtaa kwamba haki za mtoto zinavunjwa. Taarifa iwe na ushahidi kwamba mzazi, mlezi au ndugu anayemlea mtoto ana uwezo lakini anakataa au hajali kutoa chakula, malazi, haki ya kucheza au kupumzika, mavazi, huduma ya kitabibu au elimu.



(ii) Ofisa wa Ustawi wa Jamii, baada ya kupokea taarifa, atamuita mzazi au ndugu ambaye taarifa ilitolewa dhidi yake, ili kujadili suala hilo. Maamuzi yatafanywa na Ofisa wa Ustawi wa Jamii kwa ajili ya ustawi wa mtoto.

(iii) Pale ambapo mtu ambaye taarifa ilitolewa dhidi yake anakataa kutekeleza maamuzi yaliyotolewa na Ofisa wa Ustawi wa Jamii, ofisa huyo wa Ustawi wa Jamii atapeleka suala hilo mahakamani.

Mahakama itasikiliza shauri na kuhukumu suala hilo. Inaweza:

(a) Kutoa faraja au amri iliyoombwa kama mazingira yanavyohitaji; na

(b) Ikatoa amri iliyoombwa dhidi ya mzazi, na kumuamuru mzazi kutoa dhamana kama ziada ya faraja iliyotolewa ili kutoa huduma stahili na ulinzi kwa kusaini na kuahidi kumpatia mtoto lolote au mahitaji yote.

(iv) Katika sheria hii, Mahakama ya kwanza itakuwa mahakama ya kuanzia kwa masuala yote chini ya sehemu hii. Rufaa kutoka mahakama hii itafuata utaratibu wa kawaida wa rufaa.

(v) Mtu yeyote anayevunja kifungu kidogo cha (i) anatenda kosa. Akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kutumikia kifungo kwa muda wa miezi mitatu au vyote kwa pamoja.

## Uchunguzi wa Makosa Dhidi ya Mtoto

***Ulinzi wa mtoto unafatiliwa namna gani? Na nani?***

(i) Pale ambapo Ofisa wa Ustawi wa Jamii, kwa sababu za msingi, anahisi mtoto anatendewa vibaya au anahitaji huduma na ulinzi, anaweza kuingia na kukagua nyumba ambamo mtoto anatunzwa ili kuchunguza. Katika kufanya hilo, ataambatana na ofisa wa polisi.

(ii) Baada ya kuchunguza na kuonekana kuwa mtoto ametendewa vibaya au anahitaji huduma ya haraka na ulinzi, Ofisa wa Ustawi wa Jamii atamtoa mtoto na kumuweka sehemu ya usalama kwa muda usiozidi siku saba. Atamtoa mtoto akiwa na ofisa wa polisi.



(iii) Mtoto anapokuwa amewekwa sehemu nyingine, au ametolewa ili kupata huduma ya ulinzi, Ofisa wa Ustawi wa Jamii atampeleka mtoto mahakamani ndani ya siku kumi na nne kwa ajili ya amri nyingine kutolewa.

(iv) Mpaka mahakama itakapoamua suala hili, mahakama inaweza kumweka mtoto kwenye makazi yaliyoidhinishwa au chini ya malezi ya Ofisa wa Ustawi wa Jamii au kwa mtu yeyote anayefaa.

SURA 13

# MTOTO MWENYE MGOGORO NA SHERIA

## Mahakama ya Watoto

### Kuanzishwa kwa mahakama ya watoto

***Mahakama ya Watoto ina faida gani?***

(i) Kutakuwa na mahakama ya Watoto itakayokuwa na madhumuni ya kusikiliza na kuamua masuala yanayohusu watoto.

(ii) Mahakama ya Watoto itaongozwa na Hakimu Mkazi.

### Uwezo wa Mahakama ya Watoto

***Mahakama ya Watoto inafanya nini?***

(i) Mahakama ya Watoto itakuwa na uwezo wa kusikiliza na kuamua:-

(a) Mashtaka ya jinai dhidi ya watoto.

(b) Maombi yanayohusu matunzo, kukimu na kuwalinda watoto.

(ii) Mahakama ya Watoto itakuwa pia na uwezo na mamlaka iliyopewa na sheria nyingine yoyote iliyoandikwa.

(iii) Mahakama ya Watoto, pale inapowezekana, itakaa katika jengo jingine tofauti na jengo la kawaida kwa ajili ya kusikiliza kesi dhidi ya watu wazima.

## Taratibu katika Mahakama ya Watoto

***Je, taratibu za mahakama zinamlindaje mtoto akishtakiwa?***

(i) Utaratibu wa kuendesha mashauri katika mahakama ya watoto utafuata kanuni zitakazotengenezwa na Jaji Mkuu. Lakini, kwa vyovyote vile, utazingatia masharti yafuatayo:

(a) Mahakama ya Watoto itakaa mara kwa mara kufuatana na ulazima;

(b) Mashauri yataendeshwa kwa faragha;

(c) Mashauri yatakuwa ya kawaida. Uchunguzi wa mashauri utafanywa kwa njia ambayo uchunguzi hautampinga mtoto.

(d) Ofisa Ustawi wa Jamii atakuwepo wakati wa kuendesha mashauri.

(e) Ni haki ya mzazi, mlezi au ndugu kuwepo.

(f) Mtoto atakuwa na haki ya kuwa na ndugu wa karibu au kuwakilishwa na wakili.

(g) Haki ya kukata rufaa itafafanuliwa kwa mtoto ili aielewe.

(h) Mtoto atakuwa na haki ya kutoa ufafanuzi na maoni.

(ii) Pamoja na wajumbe na maofisa wa Mahakama ya Watoto, watu walio orodheshwa hapa chini wanaweza kuruhusiwa na mahakama wakati inapokaa kusikiliza shauri:



(a) Wahusika wa shauri lililopo mahakamani, mawakili wao, mashahidi, wahusika wengine wa moja kwa moja na shauri lililopo mahakamani.

(b) Mtu mwingine yeyote ambaye mahakama inaweza kumruhusu awepo mahakamani.

**Mwenendo wa Shauri katika Mahakama ya Watoto**

(i) Mahakama ya Watoto inaposikiliza tuhuma dhidi ya mtoto, itakaa katika jengo au chumba kingine tofauti na jengo au chumba ambacho mashauri ya kawaida ya mahakama husikilizwa. Kama mtoto anashtakiwa pamoja na mtu mwingine ambaye si mtoto, mashauri yatasikilizwa kwenye chumba cha kawaida cha mahakama.

(ii) Pale ambapo shauri linaendelea kusikilizwa na ikaonekana kwa mahakama kuwa mtu aliyeshtakiwa ni mtoto, mahakama itasitisha mwenendo wa mashtaka na kumpeleka mtoto kwenye Mahakama ya Watoto.

(iii) Pale ambapo shauri linaendelea kusikilizwa na ikaonekana kwa mahakama kuwa mtu aliyeshtakiwa ni mtu mzima, mahakama itaendelea kusikiliza shauri. Maamuzi yatafanywa kulingana na Sheria ya Mahakama za Mahakimu au Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka, kama itakavyokuwa.

## Dhamana kwa Ajili ya Mtoto

***Je, mtoto akikamatwa, anatendewa nini? Nani anaweza kumwekea dhamana?***

(i) Pale ambapo mtoto anakamatwa kwa hati au bila hati ya kukamata, na hawezi kupelekwa mahakamani mara moja, ofisa mkuu wa kituo cha polisi ambako amepelekwa atamwachia mtoto huru. Mtoto anaweza kujidhamini yeye mwenyewe, au kudhaminiwa na wazazi, walezi au ndugu au bila kuwa na wadhamini. Isipokuwa:

(a) Kama mashtaka ni ya mauaji au kosa ambalo adhabu yake ni kifungo kwa kipindi kinachozidi miaka saba.

(b) Kama ni lazima kwa ajili ya ustawi wa mtoto kumtoa ili asihusiane na mtu asiyefaa; au

(c) Ofisa ana sababu kuamini kuwa kumtoa mtoto kutavunja haja ya kutenda haki.

## Uhusiano na watu wazima mtoto anapokuwa kizuizini

(i) Ofisa wa Polisi atafanya mpango kwa ajili ya kuzuia, kama inawezekana kufanyika, mtoto aliye kizuizini asihusiane na mtu mzima anayetuhumiwa kutenda kosa, isipokuwa kama ni ndugu.

**Mahakama ya Watoto inaweza kusikiliza mashauri yote isipokuwa kama ni mashtaka ya mauaji**

(i) Ofisa wa Polisi hatampeleka mtoto mahakamani isipokuwa kama upelelezi umekamilika. Au kama kosa linahitaji apelekwe mahakamani.

(ii) Mtoto anapopelekwa mahakama ya watoto kwa kosa lolote lile, mahakama itasikiliza shauri hilo siku hiyohiyo, isipokuwa kwa kosa la mauaji.